JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

"Kilimani" Iringa Road,
S.L.P. 1175,
41101 DODOMA,
Barua Pepe: rbcdodoma@pccb.go.tz.
TANZANIA.

www.pccb.go.tz

DODOMA – APRILI 10, 2021

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

WAKAMATWA KWA 'KULAGHAI' AKINA MAMA

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Sheria na leo tunautaarifu umma kuhusu utendaji wetu kwa robo ya Januari hadi Machi, 2021. Lengo ni kuchagiza ushiriki wa wananchi katika mapambano dhidi ya rushwa.

Kwanza, ufuatiliaji wetu kwa njia ya udhibiti wa vitendo vya rushwa na uchunguzi wa vitendo hivyo umetuwezesha kuokoa na/au kudhibiti jumla ya shilingi milioni mia saba na nne laki moja tisini na moja mia tano themanini na mbili (704,191,582/=), nyumba moja na kiwanja kimoja, zikiwa ni mali ambazo zilichepushwa kinyume na makusudio; malipo ya tozo za halmashauri yaliyokuwa mikononi mwa watendaji; malipo zidifu yasiyo stahili; fedha zilizokuwa zichepushwe; na makato ya watumishi wa sekta binafsi ambayo hayakuwa yamewasilishwa kwenye Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (National Social Security Fund - NSSF) kwa muda mrefu.

Milioni ishirini na saba (27,000,000/=) kati ya fedha zilizookolewa zimetokana na ufuatiliaji wa miradi miwili ya maji ambapo tulibaini malipo batili kufanywa kwa wakandarasi wa miradi ya Vijiji vya Goima wilayani Chemba na Mundemu Wilayani Bahi ilihali kazi zilizoainishwa hazikufanyika. Aidha, ukaguzi maalum uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ulithibitisha mapungufu hayo

na kuelekeza, pamoja na hatua nyingine, Wakandarasi na Wasimamizi wa miradi hiyo warejeshe fedha zilizolipwa kinyume na taratibu.

Pia TAKUKURU Mkoa wa Dodoma imekuwa ikipokea malalamiko mengi kutoka kwa waajiriwa au wastaafu wa Makampuni na Taasisi binafsi wakilalamikia makato yao kutowasilishwa NSSF kwa wakati na hivyo kuwaletea usumbufu mkubwa kila wanapofuatilia mafao yao stahiki ya kisheria. Hili ni kosa la ubadhirifu kinyume na kifungu cha 28 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa [Sura 329 Marejeo 2019].

Ufuatiliaji wetu umeonyesha kwamba ni kweli baadhi ya waajiri hawawasilishi aidha sehemu au hata makato yote wanayopaswa na hivyo, kwa kushirikiana na NSSF Mkoa wa Dodoma, tumewezesha kudhibiti jumla ya shilingi milioni mia mbili kumi na nne laki moja themanini na mbili mia tano arobaini na nane (214,182,548/=) kutoka kwa waajiri thelathini (30) ambao pamoja na kukata sehemu ya mishahara ya waajiriwa wao walibaki na fedha hizo, kinyume na taratibu, bila kuziwasilisha NSSF. Ninawaasa waajiri Mkoani Dodoma kuzingatia matakwa ya kisheria na kujiepusha na vitendo hivyo.

Pili, tumekamilisha uchunguzi wa majalada 18 na kufungua mashauri mapya kumi mahakamani yaliyohusu watu binafsi na watumishi wa umma kuanzia ngazi ya Wizara hadi Mitaa. Aidha tumepokea jumla ya malalamiko 210 ambapo 108 ndiyo yaliyohusiana na rushwa. Natoa wito kwa wakazi wa Mkoa wa Dodoma kufuatilia elimu tunazotoa kwa njia mbalimbali ili wafahamu kwa undani makosa ya rushwa na wajibu wa TAKUKURU ili wawasilishe kwetu zile tu taarifa zinazohusiana na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, jambo ambalo litaongeza ufanisi kwa kutuwezesha kujikita kwenye masuala yanayotuhusu kwa mujibu wa Sheria.

Ili kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu nafasi yao katika kuzuia na kupambana na rushwa, tumeendesha semina kumi, tumetembelea na kuimarisha vilabu 73 vya wapinga rushwa, tumefanya mikutano 29 ya hadhara, tumeshiriki maonesho manne na tulielimisha kupitia vipindi vinne vya redio.

Tatu, tumeendelea kuwafuata wananchi walipo na kusikiliza kero zao ambapo kila mwezi Ofisi ya Mkoa na zote za wilaya zilitenga siku moja ya TAKUKURU INAYOTEMBEA ambapo kero zinazohusiana na rushwa zilisikilizwa na ufumbuzi wake kutolewa kwa aidha kuelimisha jamii, kudhibiti au kuzuia vitendo vya rushwa au kuanzisha uchunguzi pale ambapo taarifa za awali zinaonyesha pana viashiria vya jinai.

Nne, tunamshikilia Bw. Luka Mathayo Nkini (38) Mfanyabiashara Mkazi wa Airport Jijini Dodoma kwa tuhuma za Kujipatia Manufaa kinyume na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa [Sura 329 Marejeo 2019] ambapo tulipokea taarifa kutoka kwa Msiri wetu kwamba Mtuhumiwa akijifanya ni Mganga na 'Mjukuu wa Babu Mitimingi wa Kigoma' amekuwa akijipatia fedha na mali nyingine kutoka kwa watu mbalimbali.

Uchunguzi wetu wa awali umeonyesha kwamba Mtuhumiwa amejipatia manufaa asiyostahili kutoka kwa **akina mama kumi** ambapo alijifanya kuwa na uwezo wa kuwaongezea mara dufu fedha na vitu walivyompa. Aidha, kama sharti la kuwasaidia, amekuwa akiwataka kingono baadhi yao. Amekuwa akifanya uhalifu huo katika mikoa ya Dodoma, Arusha na Kilimanjaro.

Hadi sasa tumepata ushahidi wa Mtuhumiwa kujipatia zaidi ya shilingi milioni mia moja na tano (105,000,000/=), viwanja viwili, mashamba mawili, vifaa vya kieletroniki na fenicha na baada ya kumkamata amekiri makosa yake na kuwataja washirika wenzake katika uhalifu huo kuwa ni Bw. Hussein Hamisi Mvungi (44), Mkazi wa Himo-Kilimanjaro ambaye naye tumesha mkamata na amekiri tuhuma dhidi yake pamoja na Bw. John Gabriel Munuo, Mkazi wa Sanya-Juu Siha. Kupitia taarifa hii ninamtaka Bw. Munuo kuripoti mara moja kwenye Ofisi za TAKUKURU zilizopo karibu naye kabla ya rungu la TAKUKURU halijamfikia. Hatua stahiki za kisheria zitachukuliwa dhidi ya Watuhumiwa kulingana na ushahidi mara baada ya uchunguzi wetu kukamilika.

Mwisho, tunawasihi wananchi kuwa makini na watu wanaojifanya Maafisa wa TAKUKURU wa Mkoa wa Dodoma kwa kuwapigia simu na kuwataka aidha kuja Dodoma au kuwatumia fedha kwa njia ya simu au benki.

Huo sio utendaji wa TAKUKURU, usihadaike. Iwapo matapeli hao watawasiliana nawe usisite kutoa taarifa kwenye Ofisi yoyote ya TAKUKURU au Ofisi nyingine za umma. **RUSHWA HAILIPI.**

Imetolewa na:

Sosthenes Kibwengo
Mkuu wa TAKUKURU (M) Dodoma